

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: +25526-230081
Nukushi: +25526-2321170
Barua pepe: km@habari.go.tz
Tovuti: www.habari.go.tz



S. L. P 25,
Mtaa wa Habari,
Mji wa Serikali Mtumba,
40481 Dodoma.

TAARIFA KWA UMMA

Serikali Yaagiza Somo la Michezo Kufundishwa Shule Zote Nchini

Dodoma- Februari 09, 2021

Serikali imewaagiza Wakuu wa Shule zote za Msingi na Sekondari nchini kuhakikisha somo la michezo linafundishwa ipasavyo ili kuwaandaa vijana vyema katika michezo mbalimbali.

Azimio hilo limefikwa Februari 08, 2021 jijini Dodoma katika kikao cha pamoja kati ya Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Ofisi ya Rais TAMISEMI pamoja na Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia kilichoandaliwa na Wizara ya Habari ambacho kilijadili namna ya kuboresha michezo katika shule za msingi na Sekondari.

“Nawaagiza walimu wakuu wa shule zote nchini, kusimamia vyema vipindi vya michezo kwa kuhakikisha somo hilo linafundishwa na limeruhusiwa kuwepo kwenye mitaala na katika muda sahihi, wanafunzi washiriki vyema vipindi vya michezo. Na sisi upande wa Serikali tutasimamia vyema ajenda hiyo na tutahakikisha maafisa Elimu Mkoa na Wilaya wanafuatilia michezo katika maeneo yao,” alisema Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) Mhe. Selemani Jafo.

Mhe. Jafo ameeleza kuwa ili kuleta ufanisi katika michezo, ni wajibu kwa halmashauri zote nchini kutenga maeneo kwa ajili ya shughuli za michezo na kuwakiagiza Wakurugenzi katika halmashauri hizo kusimamia vyema miundombinu ya michezo na kuhakikisha maeneo ya michezo hayavamiwi.

Kwa upande wake Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia, Mhe. Prof. Joyce Ndalichako amesema Wizara yake inakamilisha uandaji wa michepuo ya masomo ya michezo na kuhuisha mitaala iliyopo ili somo hilo lilete tija kwa wanafunzi ambao baadhi wameanza kulifanyia mitihani katika kidato cha nne na sasa taratibu zinakamilishwa masomo hayo yaendeleo hadi kidato cha tano na sita h itakayosaidia nchi kupata wataalamu wengi zaidi.

Naye Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Mhe. Innocent Bashungwa amezishukuru Wizara hizo kwa kuzingatia dhamira ya Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Dkt. John Pombe Magufuli ni kuleta uhai katika timu za Taifa ambao unatokana na kuwepo kwa vipaji vinavyozalishwa kuanzia shule za msingi na sekondari.

Aidha, kikao pia kimeazimia kuhuisha ufanisi wa mashindano ya michezo ya sekondari na shule za msingi ikiwemo kuunda Kamati mpya ya Kitaifa na kutenga bajeti ya kutosha kwa ajili ya shughuli za michezo ya Umoja wa Michezo na Taaluma kwa shule za msingi Tanzania (UMITASHUMTA) na Umoja wa Michezo ya Shule za Sekondari Tanzania (UMISSETA)

Imetolewa na,



Eleuteri E. Mangi

**Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini
Wizara ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo**